TANGAZO LA SERIKALI NA. 217 la tarehe 29/3/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 6(1) na 16 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURUYA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara - Mikindani.

Tafsiri

3. Katika Sheria hii isipokuwa pale muktadha utahitaji vinginevyo: -

"Ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheriahii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi za wanyama hao;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo,

kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"mnada" maana yake soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"utamaduni" maana yake ni sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi, muziki wa asili, ususi, michezo, disko, muziki wa dansi, video, muziki wa taarabu, maonyesho ya sinema, mazingaombwe, tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa Ardhi" maana yake ni tozo inayotozwa kwa ajili ya mauziano ya Ardhi na mabadiliko ya Ardhi husika;

"usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya Mamlaka ya Halmashauri;

"vibao vya matangazo" maana yake ni mbao, ukuta au mahala popote na chombo chochote ambacho kimeekwa kueleza Biashara; na

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria hii;

Utozaji wa Ada na Ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni Ndogo ya

(1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni Ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni Ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria kanuni hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni Ndogo ya (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalum kuruhusu shughuli za usafirishaji wa bidhaa yoyote kufanyika nje ya muda ulioainishwa katika Sheria hii.

(6) Malipo ya ada ya huduma ya hoteli yatafanyika kuanzia tarehe 01 mpaka tarehe 07 ya kila mwezi

unaofuatia mwezi unaolipiwa ada ya huduma ya hotel.

(7) Malipo ya leseni za vileo yatafanyika kuanzia tarehe 01 mpaka tarehe 15 ya mwezi Aprili na mwezi Oktoba kila mwaka.

Utoaji wa stakabadhi za malipo

7.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria hii, utalipwa kwa Halmashauri au kwa Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Utakuwa ni wajibu wa kila mlipa ada au ushuru kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Utakuwa sio utetezi kwa mujibu wa Sheria hii, mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni Ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini (30) kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni Ndogo ya (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya

siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

9.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni Ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

(c) kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kama itakavyokubalika katika mkataba kabla ya kuanza makusanyo ambapo dhamana hiyo itarejeshwa mwisho wa mkataba.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria hii.

Mabadiliko ya Viwango vya ada na ushuru

11. Halmashauri itakuwa na uwezo wa kubadilisha viwango vya ada na ushuru pale itakapoona inafaa kwa kushirikisha Wananchi hususan wale watakaoathirika

katika utekelezaji wa marekebisho ya Sheria hii.

Wajibu wa kuzingatia Masharti ya Sheria Ndogo nyingine

12. Bila kuathiri masharti ya Kanuni ya 5, mlipa ada na ushuru atawajibika kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo nyingine zinazosimamia chanzo cha mapato ikiwa ni pamoja na wajibu wa kutumia machinjio, kutunza mazingira na usafi, kutotupa taka ovyo, au kutokiuka masharti mengine yaliyowekwa na Sheria Ndogo za Halmashauri.

Makosa

13. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria hii;

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au

(h) atatumia chombo chochote cha usafiri kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada;

(2) Itakuwa ni kosa kwa wakala: -

(a) kukusanya ada na ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba kutoka Halmashauri;

(b) kujaribu au kukusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa katika Sheria hii;

(c) kushindwa kuwasilisha au kuwasilisha pungufu ya kiwango cha ada na ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

(d) kukusanya ada na ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri.

Adhabu

14. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya Aya yoyote katika Sheria hii atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi laki mbili na kisichozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria hii kiasi cha Shilingi laki mbili (200,000) endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa T SNa. 161 la 2018

16. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ya mwaka 2018.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1)*

SEHEMU YA I: USHURU WA MAEGESHO

| Na. | Chombo cha usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Gari | 1,000.00 kwaa siku |
| 2 | Bajaji | 500.00 kwa siku |
| 3 | Pikipiki | 200.00 kwa siku |

SEHEMU YA II: USHURU WA KITUO CHA MABASI

| Na | Chombo cha usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mabasi makubwa ya abiria mikoani | 10,000.00 kwa safari |
| 2 | Mabasi madogo ya abiria | 5,000.00 kwa safari |
| 3 | Daladala nje ya mkoa/wilaya | 5,000.00 kwa safari |
| 4 | Daladala ndani ya wilaya | 1,500.00 kwa safari |
| 5 | Daladala ndani ya manispaa | 500.00 kwa safari |
| 6 | Magari binafsi | 1,000.00 kwa siku |
| 7 | Teksi | 500.00 kwa safari |
| 8 | Bajaji | 300.00 kwa safari |
| 9 | Pikipiki | 300.00 kwa safari |
| 10 | Ada ya kutunza gari lililo kamatwa au kuzuiliwa | 10,000.00 kwa siku |
| 11 | Kuingiza lori mjini | 20,000.00 kwa safari |

SEHEMU YA III:USHURU WA KUINGIZA LORI MJINI

| Na. | Chombo cha usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Tani 2 hadi 4 | 5,000.00 kwa safari |
| 2 | Tani 5 hadi 9 | 10,000.00 kwa safari |
| 3 | Tani 10 hadi 19 | 20,000.00 kwa safari |
| 4 | Tani 20 hadi hadi 30 na zaidi | 30,000.00 kwa safari |

SEHEMU YA IV: USHURU WA SOKO

| Na. | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Vibanda/maduka makubwa | 50,000/= kwa mwezi |
| 2. | Vibanda/maduka madogo | 25,000/= kwa mwezi |
| 3. | Kizimba cha matunda au mboga | 10,000/= kwa mwezi |
| 4. | Meza | 10,000/= kwa mwezi |

*Tangazo La Serikali Na. 217 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 5. | kizimba vya kuku | 10,000/= kwa mwezi |
| 6. | Kizimba cha bucha | 10,000/= kwa mwezi |
| 7. | Kizimba kuzunguka soko | 10,000/= kwa mwezi |
| 8. | Stoo/vyumba ndani ya soko | 30,000/= kwa mwezi |
| 9. | Kizimba cha tumbaku | 10,000/= kwa mwezi |
| 10. | Kizimba chenye magunia | 30,000/= kwa mwezi |
| 11. | Kizimba cha nafaka | 30,000/= kwa mwezi |
| 12. | Kizimba cha chai na chakula | 10,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA V: USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| Na. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa nyanya | 500 kwa Tenga/Boksi |
| 2. | Ushuru wa maharage | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 3. | Ushuru wa mchele | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 4. | Ushuru wa kunde | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 5. | Ushuru wa mbaazi | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 6. | Ushuru wa njugu | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 7. | Ushuru wa viazi | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 8. | Ushuru wa vitunguu | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 9. | Ushuru wa karanga | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 10. | Ushuru wa mahindi | 1,000 kwa Kilo 100 |
| 11. | Ushuru wa ndizi | 500 kwa Mkungu |
| 12. | Ushuru wa mihogo | 1,000 kwa Tenga |
| 13. | Ushuru wa kabichi | 1,000 kwa tenga |
| 14. | Ushuru wa nanasi | 1,000 kwa tenga |
| 15. | Ushuru wa nazi | 1,000 kwa kiroba |
| 17. | Ushuru wa pilipili | 1,000 kwa kiroba |
| 18. | Ushuru wa machungwa | 5,000 kwa tani |
| 19. | Ushuru wa maembe | 5,000 kwa tani |
| 20. | Ushuru wa biashara rejareja | 500 kwa siku |
| 21. | Ushuru wa biashara nyingine yeyote | 1,000 kwa Siku |

| | | |
|---|---|---|
| 22 | Kibali cha kusafirisha mazao nje ya manispaa | 200.00 kwa kilo |

SEHEMU YA VI: ADA YA UKAGUZI WA AFYA

| Na | Aina ya biashara | Ada kwa mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Baa na maduka ya vinywaji | 5,000.00 |
| 2 | Migahawa na mama lishe | 2,500.00 |
| 3 | Nyumba za wageni na hosteli | 10,000.00 |
| 4 | Kumbi za starehe au mikutano | 10,000.00 |
| 5 | Majengo mengine ya biashara | 10,000.00 |
| 6 | Eneo la kugelea | 10,000.00 |
| 7 | Eneo la kuoga | 10,000.00 |
| 8 | Eneo la chakula | 10,000.00 |
| 9 | Karakana | 10,000.00 |
| 10 | Hoteli | 20,000.00 |

SEHEMU YA VII: ADA YA KIBALI CHA USAFI WA MAZINGIRA

| Na. | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Eneo la kuogelea | 20,000.00 |
| 2. | Eneo la kuoga | 20,000.00 |
| 3. | Eneo la chakula | 30,000.00 |
| 4. | Eneo la kulala wageni | 20,000.00 |
| 5. | Karakana | 20,000.00 |
| 7. | Hoteli | 50,000.00 |
| 8 | Majengo mengineya biashara | 20,000 .00 |
| 9 | Kumbi za starehe au mikutano | 30,000.00 |
| 10 | Mama lishe | 2,500.00 |
| 11 | Baa na maduka ya vinywaji | 10,000.00 |

SEHEMU YA VIII: USHURU WA MACHINJIO

| Na. | Aina ya Mifugo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 5,000.00 kila mmoja |
| 2. | Mbuzi | 2,000.00 kila mmoja |
| 3. | Kondoo | 2,000.00 kila mmoja |
| 4. | Kibali cha kuchinja nje ya machinjio | 10,000 kwa kila mmoja |
| 5 | Ngozi | 2,000.00 kwa Ngozi moja |

*Tangazo La Serikali Na. 217 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Damu | 25,000.00 kwa mwezi |
| 7 | Pembe | 5,000.00 kwa kiroba |
| 8 | Kinyesi | 50,000.00 kwa tani |
| 9 | Kibali cha kusafirisha ngozi | 500.00 kwa kila ngozi mmoja |
| 10 | Uchinjaji wa ibada | Bure |

SEHEMU YA IX:USHURU WA UKAGUZI WA NYAMA

| Na. | Aina ya Mifugo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,000.00 kila mmoja |
| 2. | Mbuzi | 1,000.00 kila mmoja |
| 3. | Kondoo | 1,000.00 kila mmoja |

SEHEMU YA X: USHURU WA MAZAO YA UVUVI

| Na. | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Samaki kwa mnada | 5 % ya mauzo |
| 2. | Samaki kwenye kizimba | 500.00 kwa siku |
| 3. | Kizimba | 10,000.00 mwezi |
| 4. | Banda (mama lishe) | 500.00 kwa siku |
| 5. | kun'goa nanga | 5,000.00 kwa safari |
| 6. | mabanda ya wakaanga samaki | 1,000.00 kwa siku |
| 7. | madalali wa samaki | 1,000.00 kwa siku |
| 8. | wapaa samaki | 200.00 kwa siku |
| 9. | kusafirisha simbi | 15,000.00 kwa tani |
| 10. | kusafirisha vizibo | 150.00 kwa kilogram moja |
| 11. | kuingiza mazao ya uvuvi toka nje ya nchi | 200.00 kwa kilo moja |

SEHEMU YA XI: USHURU WA SHUGHULI ZA SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO

| Na. | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kibali cha sherehe za unyago, ngoma na harusi | 50,000.00 kwa sherehe |
| 2. | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | 40,000.00kwa tangazo |
| 3. | Maombi ya kibali cha kufanya Tiba za Jadi | 20,000.00 kwa tukio |
| 4. | Matamasha | 200,000.00 kwa tamasha |
| 5. | Matangazo madogo/mabango madogo | 20,000.00 kwa tangazo |
| 6. | Kupiga muziki ukumbi mkubwa | 100,000.00 kwa siku |
| 7. | Kupiga muziki ukumbi mdogo | 50,000.00 kwa siku |
| 8. | Michezo ya bahati nasibu | 10,000.00 kwa kibali |
| 9. | Mnada | 50,000.00 kwa mnada |
| 10 | Ada za washereheshaji (MC) | 20,000.00 kwa sherehe |
| 11 | Ada za wamiliki wa vyombo vya muziki | 10,000.00 kwa sherehe |

*Tangazo La Serikali Na. 217 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 12 | Uendeshaji wa ligi | 50,000.00 kwa ligi |
| 13 | Ada ya matumizi ya uwanja wa sherehe (mchana) | 200,000.00 kwa siku |
| 14 | Ada ya matumizi ya uwanja wa sherehe (usiku) | 400,000.00 kwa siku |
| 15 | Ada ya matumizi ya uwaja wa michezo | 2,500.00kwa mwezi |

SEHEMU YA XII: USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Na. | Aina ya Zao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mkaa | 500.00 kwa kiroba |
| 2. | Mbao | 500.00 kila ubao/boriti |
| 3. | Kuni | 500.00 kila mzigo |
| 4. | Nguzo | 300.00 kila moja |
| 5. | Kongoo | 200.00 kwa moja |
| 6. | Fito | 300.00 kwa mzigo |

SEHEMU YA XIII: ADA YA UZOAJI TAKA NGUMU

| Na. | Eneo | Ada kwa mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kaya moja | 2,000.00 |
| 2. | Maduka la rejareja | 5,000.00 |
| 3. | Mashine ya kukamua mafuta ya alizeti | 5,000.00 |
| 4. | Maduka la jumla | 10,000.00 |
| 5. | Migahawa | 5,000.00 |
| 6. | Mashine za kukoboa na kusaga | 10,000.00 |
| 7. | Vilabu vya pombe za kienyeji, baa, grocery, | 4,000.00 |
| 8. | Mama lishe au Baba lishe, Nyama choma au chipsi inayojitegemea | 2000.00 |
| 9. | Viwanda vya uselemala na mashine za mbao | 10,000.00 |
| 10. | Bucha (Maduka ya Nyama, samaki) | 5,000.00 |
| 11. | Nyumba za kulala wageni | 4,000.00 |
| 12. | Saluni (Ususi au Vinyozi) | 3,000.00 |
| 13. | Gereji | 10,000.00 |
| 14. | Godown (Ghala) | 7,000.00 |
| 15. | Kituo cha kuuza mafuta | 10,000.00 |
| 16. | Ofisi za Taasisi mbalimbali | 5,000.00 |
| 17. | Hoteli | 10,000.00 |
| 18 | Stoo za mkaa | 5,000.00 |
| 19 | Mafundi kushona nguo | 3,000.00 |
| 20 | Mafundi vyuma(wahunzi) | 5,000.00 |
| 21 | Kumbi za starehe, sinema | 5,000.00 |
| 22 | Majengo ya kuoshea magari au pikipiki | 5,000.00 |
| 23 | Zahanati au kituo cha afya au hospitali | 20,000.00 |
| 24 | Majengo mengine yasiyotajwa | 20,000.00 |

*Tangazo La Serikali Na. 217 (Linaendelea)*

SEHEMU YA XIV: ADA YA MFUKO WA ELIMU

| Na. | Eneo linalolipiwa Ada | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mashirika ya umma | 200,000.00 |
| 2. | Makampuni makubwa ya biashara | 200,000.00 |
| 3. | Makampuni ya simu | 400,000.00 |
| 4. | Hoteli za kitalii | 200,000.00 |
| 5. | Makampuni ya ununuzi wa korosho | 400,000.00 |
| 6. | Makampuni ya uuzaji mafuta | 300,000.00 |
| 7. | Makampuni ya uuzaji magari | 200,000.00 |
| 8. | Vituo vya redio na televisheni | 200,000.00 |
| 9. | Taasisi za kidini | 50,000.00 |
| 10. | Wafanyabiashara leseni | 100,000.00 |
| 11. | Mashamba ya chumvi | 100,000.00 |
| 12. | Vyama vya akiba na mikopo | 100,000.00 |
| 13. | Maduka ya Spea | 100,000.00 |
| 14. | Nyumba za Kulala wageni | 100,000.00 |
| 15. | Zahanati binafsi | 100,000.00 |
| 16. | Maabara | 100,000.00 |
| 17. | Gereji | 100,000.00 |
| 18. | Mabaa | 40,000.00 |
| 19. | Vituo vya Wauza Mbao | 50,000.00 |
| 20. | Wenye Mabasi | 30,000.00 |
| 21. | Wenye Malori | 40,000.00 |
| 22. | Maduka ya kuuza dawa | 20,000.00 |
| 23. | Mashine ya kukoboa na kusaga | 20,000.00 |
| 24. | Nyumba za Sinema na Video | 20,000.00 |
| 25. | Hoteli ya Migahawa | 20,000.00 |
| 26. | Maduka madogo | 10,000.00 |
| 27. | Mafundi Seremala | 5,000.00 |
| 28. | Wafanya Biashara Wadogo | 5,000.00 |
| 29. | Mafundi washonaji | 5,000.00 |
| 30. | Wafanyakazi | 5,000.00 |
| 31. | Kila Mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi. | 1,000.00 |
| 32 | Mauzo ya korosho | 20/= kwa kilo |

SEHEMU YA XV: USHURU WA MINADA YA MIFUGO

| Na. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 3,000.00 kwa kila aliyeuzwa |
| 2. | Mbuzi | 2,000.00 kwa kila aliyeuzwa |
| 3. | Kondoo au Nguruwe | 2,000.00 kwa kila aliyeuzwa |

SEHEMU YA XVI: KIBALI CHA KUKATA BARABARA

| Na. | Aina ya Shughuli | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | lami | 500,000.00 |
| 2. | changarawe | 150,000.00 |
| 3. | Vumbi | 65,000.00 |
| 4. | Kukatisha barabara kupitisha miundombinu ya maji na umeme | 50,000.00 |
| 5 | Barabara nyingine ambayo haikutajwa | 85,000.00 |

SEHEMU YA XVII: USHURU SEKTA YA UVUVI

| Na. | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Leseni ya uvuvi | 15,000.00 |
| 2. | Leseni ya vyombo vya uvuvi | 15,000.00 |
| 3. | Usajili wa vyombo vya uvuvi | 25,000.00 |
| 4. | Kusafirisha mazao bahari nje ya manispaa | 150.00 kwa kilo |
| 5. | Leseni ya kampuni inayokusanya mazao ya uvuvi | 25,000.00 |
| 6. | Leseni ya wafanyabiashara wa mazao ya bahari | 20,000.00 |

SEHEMU YA XVIII: USHURU WA KULAZA VYOMBO VYA USAFIRI

| Na. | Chombo cha Usafiri | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Magari makubwa | 5,000.00 tani 10 kuendelea |
| 2. | Magari madogo | 3,000.00 pungufu tani 10 |
| 3. | Bajaji na pikipiki | 1,000.00 |

SEHEMU YA XIX: ADA YA HUDUMA ZA AFYA

| Na. | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Usajili na kumwona daktari | 3,000 – 5,000.00 |
| 2. | Vipimo vya maabara | 5,000.00 |
| 3. | Oparesheni ndogo | 10,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Oparesheni kubwa | 150,000.00 |
| 5. | Dawa na vifaa | 1,000 - 10,000.00 |
| 6. | kulazwa | 15,000.00 |
| 7. | Vipimo maalum | 20,000.00 |
| 8. | Uchunguzi wa afya | 20,000.00 |
| 9. | Mfuko wa afya ya jamii | 30,000.00 kwa watu wasiozidi 6 |

SEHEMU YA XX: USHURU MWINGINE

| Na. | Huduma inayotolewa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Machimbo ya madini ya ujenzi | 10,000.00 Tani 4 |
| 2 | Sehemu za kufyatua tofali | 50,000.00 kwa mwezi |
| 3 | Uzio wa ujenzi | 500,000.00 |
| 4 | Faini kwa uzio wa ujenzi | 200,000.00 |
| 5 | Washauri kutoka nje | 2 % ya mkataba |
| 6 | Leseni za kumbi za sherehe | 300,000.00 |
| 8 | Uthamini maeneo ya watu binafsi | 30% ya thamani ya eneo |
| 9 | Upimaji maeneo ya watu binafsi | 30% ya thamani ya eneo |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani kwamba tarehe ..........ya Mwezi ................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya Aya ya ……..ya Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara - Mikindani ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara - Mikindani, Niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru na faini ninayodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: .....................................................
Saini: ....................................................

MBELE YA:
Jina……...............................................
Wadhifa: ..................................................
Saini: ..................................................
Tarehe: ...............................................

*Tangazo La Serikali Na. 217 (Linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya manispaa ya Mtwara- Mikindani imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika Tarehe 07 mwezi Oktoba, Mwaka 2022 mbele ya ;-

MWL. HASSAN. B. NYANGE
*Mkurugenzi wa Manispaa*
*Mtwara- Mikindani*

MHE. SHADIDA ALLY NDILE
*Mstahiki Meya wa Manispaa*
*Mtwara -Mikindani*

NAKUBALI

L.S

Dodoma,
2 February, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*